MBALIZI C.D HOSPITAL

MBALIZI EVANGELISTIC CHURCH

S. L.P 6117 P. O. Box 6117
MBEYA MBEYA
Simu +255 25 2561004/5/6 Tel. +255 25 2561004/5/6
Fax +255 25 2561006 Fax +255 25 2561006
E-mail: mbalizihospital @gmail.com

13/12/2019

TANGAZO LA KAZI

Hospitali ya Mbalizi ni hospitali teule ya Wilaya ya Mbeya na inamilikiwa na Kanisa la Uinjilisti Tanzania iliyo na makao makuu yake katika mji mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya. Hospitali inatangaza nafasi za kazi kwa kada zifuatazo;

1. **Afisa muuguzi Daraja la II (Nafasi 6)**

1.1 Sifa

Awe amehitimu stashahada (diploma)ya uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali waliosajiliwa na baraza la wauguzi na wakunga Tanzania

1.2 Kazi na Majukumu

i) Kutoa huduma za uuguzi
ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya
iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi waliochini yake
iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
v) Kutoa huduma zingine za kinga na uzazi
vi) Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi

1.3 MSHAHARA

1.4 Utalipwa mshahara wakuanzia na TGHS B

AJIRALEO.COM

2. Muuguzi Daraja la pili (Nafasi 16)

2.1 Sifa

Awe amehitimu Astashahada Uuguzi ya miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wakunga Tanzania.

2.2 Kazi na Majukumu

i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya
ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
iii) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani
iv) kutoa ushauri na saha
v) Kusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
vii) Kutoa huduma za na afya ya motto
viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
x) Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

2.3 MSHAHARA
Utalipwa mshahara kuanzia na TGHS A

AJIRALEO.COM

3. Mteknolojia Msaidizi Dawa (Nafasi 1)

3.1 Sifa

Awe amehitimu astashahada ya mteknolojia msaidizi wa dawa kwa miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na ambae amesajiliwa.

3.2 Majukumu na kazi

i) Kuandaa mahitaji na matumizi ya dawa na vifaa

ii) Kuagiza, kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
iii) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
iv) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

3.3 MSHAHARA

Utalipwa mshahara wakuanzia na TGHS A

4. Muudumu wa Afya (Nafasi 4)

4.1 Sifa

kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya

4.2 Kazi na majukumu

i) Kufanya usafi wa vifaa vya kazi,usafi wa wodi na mazingira
ii) Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwendas haja (kubwa na ndogo) na kuoha
iii) Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza
iv) Kuchukua nguo za mgonjwa kupeleka kwenda kufuliwa
v) Kuchukua sampuli za mgonjwa kwaajili ya vipimovya maabara na kufuatilia majibu
vi) Kutayarisha vifaaa kwaajili ya kusafisha na kufunga majeraha
vii) Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa
viii) Kufanya shughuli nyingine atakazo pangiwa na kiongozi wake wa kazi

4.3 MSHAHARA

Utalipwa mshahara wa kuanzia na TGHOS A

AJIRALEO.COM

5. Namna ya kuomba

Maombi yote yaambatanishwe na;

i) Maelezo binafsi (Curriculum vitae)
ii) Vyeti vilivyo thibitishwa (Certified Certificates)
A) Cheti cha taaluma pamoja na cheti cha mafunzo kwa vitendo
B) Lesseni
C) Cheti cha sekondari (kidato cha iv na kidato cha vi)
D) Cheti cha kuzaliwa
E) Kitambulisho cha NIDA/ Namba ya NIDA
F) Mwombaji awe mtanzania asiye zidi umri wa miaka 45

6. Maombi yote yatumwe kwa;

MGANGA MFAWIDHI

HOSPITALI YA MBALIZI

S.L.P 6117

MBEYA.

Barua pepe:mbalizihospital@gmail.com

SIMU 0735542568

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/01/2020 saa 9:30 Alasiri

AJIRALEO.COM